

Nyongeza 1.

Yesu katika Kurani: Orodha ya Marejeo ya Kurani kumhusu Isa (Yesu)

Yesu/Isa ndiye “**njia**” (*al sirat mustaqueem*): 43:61.

Yesu/Isa ndiye “**kweli**” (*al haq*): 19:34.

Yesu/Isa ndiye “**uzima**” (*Min Rouhina*): 21:91, 66:12

Yesu/Isa:

Alizungumza na watu akiwa mtoto kitandani: 5:110, 19:24, 19:29-33.

Mimba yake ilikuwa kwa njia ya muujiza kupitia bikira aliyeitwa Mariamu na akawako kwa neno (*fayakun*): 3:47, 3:59, 19:20.

Mimba ilikuwa kwa uwezo wa Roho wa Mwenyezi Mungu (*Rouh Al-Qudus*): 21:91, 66:12.

Yeye ni Roho wa Mwenyezi Mungu (*Rouh Allah*): 19:17, 21:91, 66:12.

Yeye ni Roho wa/aliyetoka kwa Mwenyezi Mungu (*Rouh minhu* kutoka kwa *Mwenyezi Mungu*): 4:171.

Alitiwa nguvu/aliongozwa (*ayyadhu*) na Roho Mtakatifu (*Rouh Qudus*): 2:87, 2:253, 5:110.

Yeye na Mwenyezi Mungu wote wawili wanaitwa Bwana (*rab*): 9:31.

Yeye ndiye Injili au habari njema: 3:45.

Aliteremshwa (*anzalata*) kutoka kwa Mwenyezi Mungu: 3:53.

Aliteremshwa kutoka mbinguni (hili ni fumbo katika mapokeo ya Wasufi): 5:114-115.

Yeye ndiye Neno la Mwenyezi Mungu (*kalimatu Allah*): 3:39, 3:45, 4:171.

Yohana Mbatizaji anamthibitisha Yesu/Isa kuwa ndiye “Neno”: 3:39.

Mwana aliye mtakatifu, asiye na dhambi (*zakiyyah*): 3:46, 19:19.

Hakuwa jeuri wala mwovu: 19:32.

Hakutumia mabavu wala hakuwa mnyonge (*jabbaran shakiyyan*): 19:32.

Yeye ni mwenye haki (*saliheen*): 3:46, 6:85.

Yeye yu karibu na Mwenyezi Mungu (*muqarrabeen*, yaani, yuko mahali maalumu pa heshima), yeye peke yake ndiye amepewa mahali hapo katika Kurani; 3:45.

Yeye ndiye mpatanishi/mkuu/aliyetukuzwa (*wajihan* au *wajih*) sasa na hata milele. (Hii ilikuwa ni sifa ya pekee iliyotolewa tu kwa Isa na Musa, ambao kwa namna ya kuvutia sana, walikuwa ni watu wawili wanaotoa agano [ahadi]): 3:45.

Yeye ndiye mwombezi (*shafa 'a*); haki ya pekee ya Mwenyezi Mungu aliyompa na kumhesabia Isa (kwa mujibu wa baadhi ya tafsiri za Wasufi): 2:255, 21:28.

Yeye ndiye njia iliyonyoka (*siratun mistaqueem*): 3:51, 43:61.

Amepewa siri za yale yasiyoonekana kwa macho (*ghyab*) (maajabu): 3:44.

Upendeleo wa Mwenyezi Mungu ulikuwa juu yake yeye: 5:110, 43:59.

Mwenyezi Mungu alimpa yeye “upendeleo” na hadhi ya nabii “zaidi ya wengine”: 2:253.

Mwenyezi Mungu alimbariki (*mubarak*) po pote alipokuwapo: 19:31.

Alipewa hekima na ufunuo wa Agano la Kale na Injili: 3:48, 2:36, 19:30, 43:63, 57:27.

Mwenyezi Mungu aliyadhirisha mapenzi yake kwa Yesu/Isa: 4:163.

Mwenyezi Mungu alifanya agano [ahadi] pamoja naye: 33:7.

Yeye anafanishwa na Adamu (yeye ni Adamu wa pili): 3:59.

Aliitwa Masihi: 3:45, 4:157, 4:171, 4:172, 5:17 (mara mbili), 5:72 (mara mbili), 5:75, 9:30, 9:31.

Anakuja kuithibitisha sheria: 3:50.

Amepewa mamlaka kuhalalisha vitu vilivyooharamishwa kabla: 3:50.

Yeye ni “rehema itokayo kwa Mwenyezi Mungu” (*rahmatun*): 19:21.

Alikuwa ishara dhahiri (*be-yinat*, yaani, “iliyo dhahiri na isiyo na shaka”) kwa watu (wanadamu wote): 2:87, 19:21, 21:91, 43:61.

Alionesa ishara dhahiri (*be-yinat*) za Mwenyezi Mungu: 2:253, 3:49-50, 5:114, 43:63.

Mwenyezi Mungu alimpa miujiza dhahiri: 2:253.

Alipewa uwezo wa kutia pumzi/kuumba uhai mpya kutoka katika udongo: 3:49, 5:110.

Aliwaponya vipofu na wenye ukoma: 3:49, 5:110.

Alikuwa na uwezo wa kuwafufua wafu: 3:49, 5:110.

Kwa muujiza anateremsha chakula duniani kutoka mbinguni. 5:112-118.

Watu walifanya hila (dhidi yake): 3:54.

Aliitwa “mwongo” halafu “wakamwua” (*taqutulun*): 2:8, 5:70.

Alikufa (*mutawafeka* kutokana na kitenzi cha Kiarabu *tawwafa* (kusababisha kifo) ambapo *amutu* shina lake ni *mata* (alikufa): 3:55, 4:159, 5:117, 19:33.

Alifufuliwa kutoka kwa wafu (*yum uba 'athu*): 19:33, (yawezekana 6:122).

Alipaa kwenda kwa Mwenyezi Mungu mbinguni: 3:55, 4:158.

Anarudi siku ya kiama (*yum al-qiyama*): 3:55, 4:159, 43:61.

Yeye ni ishara ya na yeye anajua siku ya hukumu: 43:61.

Ni Mjumbe/Mtume (*rasul*): 4:157, 5:75.

Yeye ni Nabii (*nabyyun*) wa Mwenyezi Mungu: 19:30.

Yeye ni mtumishi (*abd Allah*) wa Mwenyezi Mungu: 4:172, 19:30, 43:59.

Yeye ni Shahidi (*shahid*) mwaminifu wa Mwenyezi Mungu: 4:159, 5:117.

Amani (*salaam*) i juu yake: 19:33.

Yeye ni kielelezo kwa wana wa Israeli: 43:59.

Aliwatia moyo wanafunzi (*al-hawariyun*) kuwa na imani kwa Mwenyezi Mungu: 5:111.

Wanafunzi ni wasaidizi wa Mwenyezi Mungu (*ansar Allah*) wanaomtangaza Yesu/Isa: 3:52, 61:14.

Wanafunzi wake wanayo mamlaka dhidi ya adui zao: 61:14.

Wanafunzi ni mashahidi wa ukweli wa Yesu/Isa: 5:113.

Sisi tunaagizwa kumtii yeye (*atee 'uon*): 3:50, 43:63.

Tunaagizwa kumwamini yeye (*aamanou*): 4:159, 5:110.

Tunaagizwa kumfuata (*ettabio 'un*) yeye: 3:55, 43:61.

Wafuasi wake wako juu (*fawqua*) ya wale wasioamini: 3:55.

Wafuasi wake wanakubalika (ni waumini wa kweli) (*aamanou minhum*) kwa Mwenyezi Mungu: 57:27.